

SHULE YA SEKONDARI SIMBAY

S. L. P 266

Barua pepe .....

Mobil 0717507559/0693317780

Tarehe .....

Kumb Na .....

Jina la Mwanafunzi .....

.....

S.L.P .....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI **SIMBAY** WILAYA YA **HANANG** MKOA WA **MANYARA** MWAKA **2021**.

**1.0** Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka **2021**. Shule ya sekondari **Simbay** ipo umbali wa **km 35** kusini mji mkuu halmashauri ya **Hanang**. Usafiri wa basi kutoka mjini **upo** unapatikana katika kituo cha mabasi cha **Katesh**. Nauli ni **Tsh 3000**. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe Kimi na moja **(11) Januari 2021**. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01 /2021**na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** ndani ya siku saba.

## **2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia**

### **2.1 Sare za shule**

- (a) Sare ya shule hii, ni **KUJANI( sweta na sketi au suruali zote rangi moja}** kwa wavulana **suruali mbili na mashati mawili meupe ya mikono mifupi** na wasichana **siketi mbili na mashati mawili ya mikono mifupi.kitambaa kizito**  
Suruali iwe ina marinda mawili na isiwe ya kubana yaani modo haitakiwi . Pia wasichana sketi zao ziwe ndefu zinazofika chini ya goti inchi nne (4) kutoka magotini, na marinda 12, sio rinda boksi. Naambatanisha kipande cha kitambaa kinachohitajika pamoja na fomu hii.
- (b) Rangi ya hijab ni nyeupe
- (c) Sare za michezo kwa shule hii ni bukta nyekundu kwa **wavulana** tisheti nyekundu. **Wasichana** bukta nyeupe na tisheti nyekundu.

**2.2** Daftari kubwa 9 na ndogo 9 kwa ajili ya mazoezi , kalamu ya wino na kalamu ya lisasi za kutosha na mkebe wa hesabu,begi kubwala mgongoni na sio lastiki/BOBMALLY hairuhusiwi.

**2.3 Shule ni ya kutwa**, chakula cha wanafunzi kinapatikana kutoka katika michango ya wazazi. Mzazi anachangia debe tatu (3) mahindi, maharage ni debe (1) pamoja na fedha kiasi cha shilingi thelathini na moja elfu (**31,000/=**) kwa mwaka, hivyo mzazi anatakiwa kufikisha michango ya chakula mtoto anaporipoti shuleni mapema .

### **3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya waziri mkuu- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- (a) Heshima kwa viongozi , wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- (c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- (g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- (i) Kutunza mali za umma.

### **3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule au kusimamishwa shule;**

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na ushoga
- (c) Ubakaji
- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi kubeli na kadhalika
- (e) Kupigana au kupiga
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- (g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- (h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
- (i) Kuoa au kuolewa
- (j) Kutoa mimba
- (k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- (l) Kukataa adhabu kwa makusudi /kugomea adhabu.
- (m) Kuwa na simu ya mkononi,laini,chaja,betri,headphone na vifaa vingine vya simu.

### **4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi;**

- (a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa mengine
- (c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- (d) Pia mwanafunzi atatakiwa kuleta jembe moja pamoja na mpini wake na kukabidhi kwa mwalimu wa vifaa.
- (e) Mwanafunzi atatakiwa kuleta slesha (fekeo) moja nakukabidhi kwa mwalimu wa vifaa kwa ajili ya usafi wa mazingira ya shule.

**5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

.....

**MKUU WA SHULE**